TANGAZO LA SERIKALI Na. 15 la tarehe 3/1/2025

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli iliyokusudiwa chini ya Sheria Ndogo hii;

"machinjio" maana yake ni sehemu inayomilikiwa na taasisi ya umma au mtu binafsi iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia mifugo;

"meneja wa machinjio" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia machinjio;

"mifugo" maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, mbwa, paka, kuku na inajumuisha ndege na wanyama wengine wanaofugwa na binadamu;

"mkaguzi wa nyama" maana yake ni mtaalam wa afya ya

mifugo aliyeajiriwa na Serikali na kusajiliwa au kuorodheshwa au kuandikishwa na Baraza la Veterinari Tanzania;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mmiliki wa machinjio" maana yake ni mtu anayemiliki machinjio binafsi katika eneo la Halmashauri;

"msafara wa mifugo" maana yake ni kundi au makundi ya mifugo yanayosafiri kutoka eneo moja kwenda eneo jingine;

"njia ya mifugo" maana yake ni njia iliyotengwa mahususi kwa ajili ya kupitisha mifugo;

"ufugaji wa ndani" maana yake ni ufugaji na ulishaji wa mifugo ndani ya jengo, zizi au eneo lenye uzio;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi cha watu, kampuni au taasisi, iliyoingia mkataba kutekeleza jukumu lolote chini ya Sheria Ndogo hii kwa niaba ya Halmashauri;

"zizi" maana yake ni jengo au eneo lililozungushiwa uzio ambalo linatumika kuhifadhi mifugo iliyokamatwa ambalo litatunzwa na kusimamiwa na Halmashauri.

Wajibu wa Halmashauri

**4**. Halmashauri itakuwa na wajibu wa-

(a) kusimamia maandalizi na utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji;
(b) kuelekeza idadi ya mifugo ambayo kila mfugaji anaruhusiwa kufuga kulingana na ukubwa wa eneo;
(c) kujenga majosho ya mifugo kwa kushirikiana na wananchi;
(d) kutoa elimu ya ufugaji bora kwa jamii kwa ajili ya kuongeza tija;
(e) kufanya sensa ya mifugo, kuweka alama na kutoa kadi za mifugo;
(f) kutoa chanjo kwa kushirikiana na wafugaji kwa ajili ya kudhibiti magonjwa ya mifugo; na
(g) kudhibiti mifugo inayozurura katika eneo la

Halmashauri.

Wajibu wa mfugaji

**5**.-(1) Kila mfugaji atakuwa na wajibu wa kuzingatia masharti ya ufugaji yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1), kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hii atahakikisha kuwa:

(a) anafuga kwa kuzingatia mipango ya matumizi bora ya ardhi kama ilivyoainishwa na Halmashauri kwa kuzingatia kanuni ya 4 ya Sheria Ndogo hii;
(b) anafanya ufugaji wa ndani kulingana na maelekezo yaliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii;
(c) analisha na kunywesha mifugo anayomiliki kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji;
(d) anahudhuria mafunzo ya ufugaji bora;
(e) anadhibiti magonjwa ya wanyama kwa kuogesha na kuipatia chanjo mifugo;
(f) mifugo inawekewa alama maalumu kwa ajili ya utambuzi;
(g) anakuwa na kadi ya mifugo itakayoonesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
(h) anapata kibali cha kusafirisha mifugo na mazao ya mifugo iwapo anahitaji kusafirisha mifugo au mazao ya mifugo; na
(i) anauza mifugo katika soko, mnada au gulio.

Kibali cha kufuga wanyama

**6**.-(1) Mtu yeyote atakayetaka kufuga mifugo atalazimika kupata kibali cha kufuga kutoka kwa Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Kibali kilichotajwa katika kanuni ndogo ya (1) hakitakuwa na gharama na kitakua cha miaka mitatu kuanzia tarehe kilipotolewa.

(3) Halmashauri inaweza kufuta kibali cha kufuga iwapo mfugaji atakiuka masharti ya ufugaji yaliyoainishwa katika kanuni ya tano ya Sheria Ndogo hii.

(4) Mfugaji aliyefutiwa kibali cha kufuga anaweza kuomba kibali upya kwa Halmashauri baada ya

kurekebisha kasoro zilizosababisha ukiukaji wa masharti ya kibali.

Masharti ya Ufugaji

**7**. Mfugaji hataruhusiwa-
(a) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa shughuli hiyo;
(b) kusafirisha mifugo kwa kuswaga barabarani;
(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;
(d) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;
(e) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au magulio ya mifugo yaliyoidhinishwa bila kibali maalum cha Halmashauri;
(f) kufuga mifugo zaidi ya idadi iliyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; au
(g) kununua, kuuza au kufanya Biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo na Halmashauri.

Kibali cha kusafirisha mifugo

**8**.-(1) Mtu ambaye anataka kusafirisha mifugo na, au mazao ya mifugo kutoka au kuingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali maalumu kilichoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria ndogo hii.

(2) Halmashauri itatoa kibali cha kusafirisha mifugo baada ya mfugaji kutoa uthibitisho wa kumiliki mifugo ikiwa na afya nzuri, imeogeshwa na kupatiwa chanjo kabla ya kusafirishwa.

(3) Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukamata mifugo inayosafirishwa bila kibali.

Kudhibiti mifugo inayozurura

**9**.-(1) Kila mfugaji atakuwa na wajibu wa kuzuia au kudhibiti mifugo kuzurura katika maeneo ambayo

hayakutengwa kwa ajili ya malisho na ufugaji.

(2) Kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji ulioandaliwa, Halmashauri itadhibiti mifugo inayozurura katika maeneo ambayo hayakupangwa kwa matumizi hayo.

(3) Endapo mifugo iliyokamatwa haitachukuliwa na mfugaji ndani ya siku saba kuanzia kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya mahakama, na fedha zitakazopatikana zitakabidhiwa kwa mmliki wa mifugo baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mifugo, gharama ya mahakama na gharama ya mnada.

(4) Mmiliki wa mifugo iliyokamatwa atatakiwa kulipa faini ya Shilingi elfu kumi (10,000) kwa siku kwa kila mfugo aliyekamatwa.

(5) Kabla ya kuuza mifugo kwa mnada, Halmashauri itatoa taarifa ya siku tatu kwa mmiliki na umma kuhusu kusudio hilo.

(6) Baada ya mauzo, Halmashauri itakata fedha ya faini, gharama za utunzaji, gharama za mnada na gharama za kesi. Fedha zitakazobakia atapewa mmiliki wa mfugo.

(7) Endapo mifugo itakufa kutokana na sababu yoyote, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama isipokuwa kama kifo kimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri.

Ukaguzi wa mifugo na mazao ya mifugo

**10**.-(1) Afisa mwidhiniwa anaweza kukagua mifugo au mazao ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri na anaweza kukataa aina yoyote ya mifugo au mazao ya mifugo kuingia au kuuzwa ndani ya eneo la Halmashauri, iwapo atakuwa na sababu za msingi za kuamini kwamba mifugo au mazao ya mifugo yanaweza kuhatarisha afya au usalama wa mifugo mingine au watumiaji.

(2) Afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika nyumba au jengo lolote kati ya saa kumi na mbili kamili asubuhi na saa kumi na mbili kamili jioni kwa lengo la

utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Operesheni maalum ya ukaguzi wa mifugo

**11**. Kutakuwa na operesheni maalumu itakayoandaliwa na Halmashauri kwa kushirikiana na wataalamu pamoja na wadau wengine kutoka katika vyombo vya usalama kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji, ukaguzi, au ukamataji wa mifugo inayozurura au inayofugwa bila kuzingatia matakwa ya Sheria Ndogo hii.

Taratibu za biashara ya mifugo na mazao ya mifugo

**12**.-(1) Kabla ya kuanza biashara ya mifugo na mazao ya mifugo, mfanyabiashara atatakiwa kuwa na leseni, utambulisho na vibali kutoka mamlaka husika vinavyohusu kuuza na kununua mifugo na mazao ya mifugo na atatakiwa kuwasilisha vibali vyake Halmashauri kwa ajili ya uhakiki.

(2) Mfanyabiashara wa mifugo inayopelekwa au kutoka mnadani au machinjioni atatakiwa kuwa na kibali kutoka Halmashauri.

(3) Mfanyabiashara atakayesafirisha mifugo kutoka nje ya Halmashauri atatakiwa kuwa na kibali kutoka Halmashauri ambayo mifugo hiyo inatoka.

(4) Mfanyabiashara wa mifugo atatakiwa kusafirisha mifugo katika vyombo vya usafiri vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria.

(5) Mifugo itauzwa au kununuliwa katika minada na masoko yanayotambulika kwa mujibu wa sheria.

(6) Minada ya mifugo au magulio ya mifugo itafanyika kwa kibali maalumu cha Halmashauri na kwenye maeneo yaliyoruhusiwa.

Bucha au duka la nyama

**13**. Mfanyabiashara wa bucha au duka la nyama atahakikisha -

(a) anamiliki leseni na vibali vya kufanya biashara hiyo;
(b) anatumia kabati la vioo la kuzuia inzi na wadudu wengine wataambao;
(c) anaweka pipa la kuhifadhia taka ngumu na laini;
(d) anaweka jokofu la kuhifadhia nyama;
(e) jengo la biashara lina mwanga wa kutosha,

umeme, maji safi na salama, visu, meza, mzani wa kawaida au mzani wa kielektroniki, na misumeno maalumu ya kukatia nyama;

(f) nyama imekaguliwa na mkaguzi aliyeidhinishwa na kugongwa muhuri;

(g) muuzaji anavaa sare nyeupe muda wote ambazo ni mabuti, koti na kofia;

(h) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita na kuhakikisha anakuwa na cheti cha upimaji;

(i) anatoa ushirikiano kwa wakaguzi mara atakapotakiwa kufanya hivyo wakati wowote wa ukaguzi;

(j) anatambuliwa na kusajiliwa na mamlaka nyingine husika za Serikali kwa mujibu wa sheria; na

(k) biashara ya nyama inafanyika katika bucha na maduka maalumu.

Usafirishaji wa nyama

**14**.-(1) Mfanyabiashara wa nyama atatakiwa kusafirisha nyama kutoka machinjioni kwa kutumia gari maalumu na endapo atatumia usafiri wa pikipiki au baiskeli atatakiwa kubeba nyama kwa kutumia chombo maalumu kilichoainishwa na Halmashauri.

(2) Kila mmiliki au mtumiaji wa gari la kubeba nyama atahakikisha kuwa gari-

(a) limesajiliwa na kupewa cheti maalumu cha ukaguzi na Halmashauri;

(b) linakaguliwa kila baada ya miezi mitatu;

(c) lina sanduku la aluminiamu lenye mfuniko na limepakwa rangi nyeupe, mstari mwekundu na namba;

(d) halibebi kitu kingine tofauti na nyama; na

(3) Kila mmiliki au mtumiaji wa gari la kubeba nyama atapaswa kulipia gharama za usafirishaji zilizowekwa na Halmashauri.

Kuingiza wanyama katika machinjio

**15**.-(1) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atakuwa na wajibu wa kuhakikisha umiliki wa mnyama anayekusudiwa kuchinjwa unathibitishwa kabla ya kuingizwa katika eneo la machinjio.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1),

meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atakagua kibali cha usafirishaji wa mnyama na nyaraka nyingine zinazothibitisha umiliki.

(3) Meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio atatunza rejista ya wanyama waliopokelewa machinjioni ambayo itaainisha aina ya mnyama, jinsi, umri na taarifa za mmiliki

Taratibu za kutembelea eneo la machinjio

**16**. Mtu anayetaka kutembelea eneo la machinjio, iwapo mtu huyo hahusiki na shughuli za kila siku katika machinjio, atatakiwa kuomba kibali kwa maandishi kabla ya siku ya kutembelea na meneja wa machinjio au mmiliki wa machinjio anaweza kumruhusu mtu huyo na kumtaka kuvaa mavazi maalum yanayopatikana katika eneo la machinjio.

Ukaguzi wa wanyama

**17**.-(1) Mkaguzi wa nyama atakagua mfugo unaoingizwa katika machinjio kwa ajili ya kuchinjwa.

(2) Endapo mfugo utagundulika kuwa na magonjwa hatarishi kwa afya ya binadamu, mkaguzi atamhifadhi katika eneo maalum kwa ajili ya matibabu au taratibu nyingine.

Sura ya 156

(3) Kabla ya mnyama kutengwa, taratibu zilizoainishwa katika Sheria ya Magonjwa ya Wanyama zitafuatwa.

(4) Endapo mnyama aliyetengwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2) ataendelea kuwa na magonjwa yaliyosababisha atengwe, afisa mwidhiniwa atamtaka mmiliki wa mnyama huyo kumtoa nje ya eneo la machinjio kwa matibabu zaidi.

(5) Endapo mmiliki atashindwa kumwondoa mnyama aliyetengwa ndani ya muda wa saa kumi na mbili tangu kutolewa kwa maelekezo ya kuondolewa, afisa mwidhiniwa anaweza kuamuru mnyama huyo kuteketezwa kwa gharama ya mmiliki.

(6) Afisa mwidhiniwa atakuwa na wajibu wa kuchukua kumbukumbu za mmiliki na mnyama aliyebainika kuwa na magonjwa na kumweka alama maalum itakayomtambulisha mnyama huyo.

Udhibiti wa shughuli za machinjio

**18**.-(1) Meneja au mmiliki wa machinjio atahakikisha kuwa shughuli za machinjio zinaendeshwa

kwa kuzingatia sheria na taratibu za afya ikiwa ni pamoja na-

(a) watoa huduma kupima afya kila baada ya miezi mitatu;

(b) watoa huduma kuwa wasafi na kuvaa mavazi maalumu kwa ajili ya kazi hiyo;

(c) kutoruhusu mkusanyiko isipokuwa kwa kibali maalumu kitakachotolewa na Halmashauri;

(d) kutoruhusu kufanyika biashara nyingine yoyote katika eneo la machinjio.

(2) Mtu hataruhusiwa kuweka bucha, duka la nyama au biashara yoyote ya nyama ndani ya mita mia mbili kutoka eneo la machinjio.

(3) Mfanyabiashara ya nyama anapaswa kuwa amesajiliwa na Bodi ya Nyama na awe na leseni ya biashara.

(4) Mtu hataruhusiwa kuchinja mifugo bila mifugo hiyo kufanyiwa ukaguzi.

(5) Itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja mifugo mahali pengine ambapo sio machinjio isipokuwa kwa kutoa taarifa kwa afisa mwidhiniwa.

(6) Mtu yeyote hatoruhusiwa kuingiza mifugo katika machinjio kwa ajili ya kuchinja baada ya saa kumi na moja kamili jioni isipokuwa kwa kibali cha Halmashauri.

(7) Mtu hataruhusiwa kutoa mifugo hai, iliyokufa au nyama nje ya eneo la machinjio bila ya idhini ya maandishi ya meneja au mmiliki wa machinjio.

(8) Haitakuwa ruksa kwa mtu mwenye majeraha, michubuko au ugonjwa unaoambukiza kwa njia ya hewa au kugusana kuingia katika eneo ya machinjio au eneo la uzalishaji wa nyama isipokuwa kwa kibali cha daktari.

Ukaguzi wa nyama

**19**.-(1) Mkaguzi wa nyama atakuwa na wajibu wa kukagua nyama katika eneo la machinjio baada ya mnyama kuchinjwa kwa ajili ya kubaini ubora wa nyama kwa matumizi ya binadamu.

(2) Endapo itabainika kuwa nyama iliyokaguliwa-

(a) inafaa kwa matumizi ya binadamu, mkaguzi

wa nyama atagonga nyama hiyo muhuri unaothibitisha kuwa nyama iliyokaguliwa ni salama kwa matumizi ya binadamu; au

(b) haifai kwa matumizi ya binadamu, nyama hiyo itateketezwa kwa kuchomwa moto au kwa njia nyingine itakayoonekana inafaa na mkaguzi wa nyama atachukua kumbukumbu za nyama hiyo na za mmiliki wake.

(3) Endapo matokeo ya vipimo vya awali yatakuwa na mashaka kuhusu ubora wa nyama kwa matumizi ya binadamu, mkaguzi wa nyama atahakikisha kuwa nyama husika inahifadhiwa kwa muda usiozidi saa ishirini na nne ili kuruhusu vipimo zaidi vya kimaabara kufanyika.

(4) Meneja au mmiliki wa machinjio atatunza rejesta ya nyama zilizokaguliwa ambayo itaonesha aina ya nyama, jinsi, umri, uzito na taarifa za mmiliki na kama nyama inafaa au haifai kwa matumizi ya binadamu.

Rejesta ya mifugo

**20**. Meneja au mmiliki wa machinjio atakuwa na wajibu wa kutunza rejesta ya mifugo iliyochinjwa na ambao haijachinjwa ikionesha aina, jinsi, umri, uzito wa mfugo, na jina na anwani ya mmiliki wa mfugo.

Udhibiti wa ufugaji wa mbwa

**21**.-(1) Mtu anayefuga au anayekusudia kufuga mbwa atapaswa kutoa taarifa kwa Halmashauri kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya umiliki wa mbwa huyo.

(2) Mfugaji atawajibika kumpatia chanjo mnyama wake na kulipa ada ya chanjo kama atakavyoelekezwa na Halmashauri.

(3) Mfugaji atawajibika kuhakikisha mbwa anayemfuga hazururi na kuleta madhara kwa wakazi wengine.

(4) Mfugaji atawajibika kuogesha mbwa ili kudhibiti magonjwa na wadudu wasumbufu.

(5) Mfugaji atalazimika kumfunga mbwa kwa mnyororo maalumu wakati wa kutembea nae kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine kwa mujibu wa Sheria.

(6) Endapo mfugaji anakusudia kusafirisha mbwa atalazimika kuwa na kasha maalumu.

(7) Halmashauri inaweza kumkamata na kumhifadhi kizuizini kwa muda usiozidi siku saba mbwa anayezurura, na iwapo baada ya muda huo kupita pasipo mmiliki kutambulika, Halmashauri inaweza kuchukua hatua nyingine kadri itakavyofaa.

Uanzishwaji wa kilimo cha ufugaji wa samaki

**22**. Halmashauri itahakikisha-

(a) inahamasisha wananchi juu ya uanzishaji wa kilimo cha ufugaji wa samaki;

(b) inaanzisha mabwawa ya mfano ya samaki katika kila kata;

(c) inawezesha upatikanaji wa Maafisa Ugani wa Uvuvi kwenye kata na vijiji;

(d) inaanzisha kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki ili kurahisisha upatikanaji pindi wafugaji wanapohitaji kununua; na

(e) inashirikiana na wadau, mashirika na taasisi mbalimbali kwa ajili ya uanzishaji wa miradi ya ufugaji samaki na tafiti za samaki.

Kibali cha kutoa huduma za mifugo

**23**. Mtu yeyote ambaye anataka kutoa huduma za mifugo kwa kuanzisha duka la kuuza vyakula vya mifugo, ghala la kuhifadhia vyakula vya mifugo, kiwanda cha kutengeneza vyakula vya mifugo, vituo vya huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga katika eneo la Halmashauri atalazimika kuwa na kibali maalumu kitakachoruhusu kutoa huduma hiyo kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Makosa

**24**. Mtu anatenda kosa endapo-

(a) atashindwa au kukataa kuogesha au kuchanja mfugo au mifugo yake ili kuzuia magonjwa;

(b) atalisha mifugo kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;

(c) ataingiza mifugo kutoka nje ya Halmashauri bila ya kibali;

(d) ataanzisha duka la kuuza vyakula vya mifugo, ghala la kuhifadhia mifugo, kiwanda cha kutengeneza vyakula vya mifugo, vituo vya

huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga bila kuwa na kibali kutoka Halmashauri;

(e) atashindwa au kwa makusudi hatatoa taarifa juu ya uwepo wa au dalili za ugonjwa au kifo cha ghafla cha mfugo au mifugo katika banda lake;

(f) atashindwa kuwasilisha taarifa ya mwezi ya uuzaji wa vyakula vya mifugo, utengenezaji wa vyakula vya mifugo au ghala, vituo vya huduma za mifugo au zahanati na vituo vya kutotolesha vifaranga;

(g) atauza au kufuga mifugo sehemu ambayo haijaruhusiwa;

(h) ataruhusu mifugo kuzurura;

(i) atakataa kutoa ushirikiano wa uwekaji wa alama kwa mifugo; au

(j) atamzuia Mkurugenzi, afisa mwidhiniwa, mkaguzi wa nyama, meneja au mmiliki wa machinjio kutekeleza majukumu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Adhabu

**25**. Mtu akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichopungua miezi sita jela na kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja

Kufililisha kosa

**26**. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2)(b))*

MAELEKEZO KUHUSU UFUGAJI WA NDANI

| Namba | Aina ya mifugo | Idadi | Maelekezo |
|---|---|---|---|
| 1. | | | |
| 2. | | | |
| 3. | | | |

**Maelekezo yajikite kueleza aina ya mifugo, idadi kulingana na ukubwa wa eneo, mila na desturi za wakazi wa eneo husika kwa kuzingatia adha inayoweza kusababishwa na ufugaji**

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(1))*

### KIBALI CHA KUFUGA MIFUGO

Jina la Mfugaji:………………………………………………………..
Anuani:…………………………………………………………...........
Kata:……………………………………........Kijiji:………………….........
Namba ya  Nyumba:………………………. Namba ya Kitalu:……………...
Ameruhusiwa kufuga Mifugo ifuatayo katika eneo la ………….........

| Namba | Aina ya Mfugo | Koo | Idadi ya Mifugo | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Jike | Dume | |
| 1. | Ng'ombe | | | | |
| 2. | Mbuzi | | | | |
| 3. | Kondoo | | | | |
| 4. | Nguruwe | | | | |
| 5. | Ngamia | | | | |
| 6. | Punda | | | | |
| 7. | Paka | | | | |
| 8. | Farasi | | | | |
| 9. | Sungura | | | | |
| 10. | Mbwa | | | | |
| 11. | Kuku/Bata | | | | |
| 12. | Wanyama wengine | | | | |

Kibali hiki kimetolewa kwa ndugu……………………………………leo tarehe…………na kitamaliza muda wake tarehe ….……………….

Kimetolewa na:
Jina..........................................................................................................
Saini………..............................................................................................
Wadhifa: ……………………………………………………………....
Tarehe: …………………...........................................................................
Muhuri: ………………………………………….......................................

## JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 8(1))*

A. KIBALI CHA KUSAFIRISHA MIFUGO

Jina:…………………………………………….
Anuani:…………………………………………
Ameruhusiwa kusafirisha mifugo ifuatayo kutoka ………………kupitia njia za……………………..hadi…………..…..

| | Aina ya mifugo | Idadi ya Mifugo |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | |
| 2. | Mbuzi | |
| 3. | Kondoo | |
| 4. | Nguruwe | |
| 5. | Ngamia | |
| 6. | Punda | |
| 7. | Paka | |
| 8. | Farasi | |
| 9. | Sungura | |
| 10. | Mbwa | |
| 11. | Kuku/Bata | |
| 12. | Wanyama wengine | |

Kibali hiki kitakuwa cha muda wa siku…....... kuanzia tarehe…..........hadi tarehe……….

Kimetolewa na :
Jina:……………………………………….
Saini:………………………………………
Wadhifa:……………………………………
Tarehe:………………………………………
Muhuri:………………………………………

B. KIBALI CHA RUHUSA YA KUINGIZA MIFUGO KATIKA ENEO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILWA

| Na | Aina ya mnyama | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Ng'ombe | |
| 2 | Mbuzi | |
| 3 | Kondoo | |
| 4 | Nguruwe | Kundi moja |
| 5 | Ngamia | |
| 6 | Punda | |
| 7 | Paka | |
| 8 | Farasi | |
| 9 | Sungura | Kundi moja |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | Mbwa | |
| 11 | Kuku /Bata | Kundi moja |
| 12 | Wanyama wengine | Kulingana na aina ya wanyama husika |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 26)*

FOMU YA KUKIRI KOSA

Mimi………………………………………………………NAKIRI KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya .…… ya Sheria Ndogo ya Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ya Mwaka 2024.

NAKUBALI kulipa ada ninayodaiwa ya kiasi cha shilingi .................... pamoja na faini ya kufifilisha kosa ya kiasi cha shilingi ......................

NATHIBITISHA KWAMBA, maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa MIMI MWENYEWE na kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu.

Leo hii tarehe………….ya mwezi…………..… mwaka 20…………….
Jina………………………………......
Saini……….......………………......

MBELE YA MKURUGENZI

Jina:………………….....................................
Saini:…………………..…..............................
Tarehe:..............................................................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa uliofanyika tarehe 9/11/2023 mbele ya-

HANAN M. BAFAGHI,
*Mkurugenzi Mtendaji (W),*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa*

MHE. ISSA B. MATEKA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri Ya Wilaya Ya Kilwa*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
29 Agosti, 2024.

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*